Je, Sheria ya Haki Mayumba ni nini?

Mnamo 1968, Sheria ya Haki Mayumba (FHA) ilitiwa sahihi, na kufanya kuwa kinyume cha sheria kwa watu kubagua katika nyanja yoyote ya makazi kwa kutegemea ukabila, rangi, asili ya kitaifa, dini, kinsia, hali ya kifamilia na ulemavu. FHA hufafanua haya kama kategoria zake saba zinazolindwa na sheria y a shirikisho.

Mahali ambapo Sheria ya Haki Mayumba Hutumika

Sheria ya Haki Mayumba hutumika wakati watu wanakodisha au kununua nyumba, kuchukua rahani, kutafuta usaidizi wa makazi, au kushiriki katika miamala mingine yoyote inayohusiana na makazi.

JE, UNAJUA KUWA UNAWEZA KUWASILISHA LALAMIKO?

WASILIANA NASI

Tutajibu ndani ya siku 1 ya kazi na kuelekeza lalamiko lako kwa wakala anayefaa.

SIMU YA LALAMIKO:
520-306-0938
hotline@seriaz.org
Biashara Inayotumia Mawasiliano ya Relay ya AZ

Nyenzo hii inategemea kazi inayoungwa mkono na Idara ya Makazi na Maendeleo ya Miji (HUD) chini ya Ufadhili wa FHIP EOI FEOI20038 na FEO2100215.

Maoni yoyote, utambuzi na mahitimisho au mapendekezo yaliyotolewa katika nyenzo hii ni ya waandishi na sio lazima kuwa yanaakisi mitazamo ya HUD.

seri

Kusaidia jumuiya za Southwest tangu 1994.

Elimu ya Haki Mayumba

seriaz.org/fair-housing/swahili/

3202 E. Grant Rd., Tucson, AZ 85716

seri

Kusaidia jumuiya za Southwest tangu 1994.

Historia

Ilianzishwa mwaka wa 1994. Sonora Environmental Research Institute, Inc. (SERI) ni shirika la ndani lisilo la faida linalopatikana Tucson, Arizona linaloshirikiana na jumuiya zenye mapato duni na za watu wachache ndani ya Southwest ili kusaidia kulinda mazingira na kuboresha afya ya jamii. Kupitia kwa msaada na elimu, SERI inaisaidia jumuiya kuangamiza ubaguzi wa makazi na kulinda haki za wote katika haki mayumba.

SERI huelekeza malalamiko kwa mshirika ambaye ni wakala wa eneo, Southwest Fair Housing Council (SWFHC), ambaye atawasaidia wateja kuhusu madai ya ubaguzi haramu wa makazi kwa kutoa usaidizi wa upelelezi, ushauri, na kupunguza athari za malalamiko, na kuelekezwa kwa rasilimali ndani ya Arizona.

Ni nini kimepigwa marufuku?

- Kukataa kukodisha, kuuza au kujadiliana kuhusu makazi.
- Vinginevyo kufanya makazi kutopatikana au kukatisha mtu tamaa ili asinunue au kukodisha nyumba.
- Kuweka sheria tofauti, masharti au haki za kuuza au kukodisha nyumba.
- Kutoa haki tofauti au kuzuia haki kwa mtu katika huduma za makazi au nyenzo za nyumba.
- Kukataa kwa uongo kuwa makazi hayapatikani ili kuangaliwa, kuuzwa au kukodishwa.
- Kutoa tangazo la nyumba linaloashiria mapendeleo yoyote, uzuiaji au ubaguz.
- Kuweka bei tofauti za kuuza au ada za kukodisha kwa kuuza au kukodisha nyumba.
- Kutumia vigezo tofauti vya kustahiki au matumizi, au viwango vya kuuza au kukodisha au taratibu.
- Kumsumbua mtu.
- Kutoa sehemu fulani ya jengo au ujirani kwa mtu.
- Kukataa kutoa mkopo wa rahani au kutoa usaidizi mwingine wa kifedha kwa ajili ya nyumba.
- Kukataa kutoa maelezo kuhusu mikopo.
- Kuweka sheria na masharti tofauti kwa mkopo, kama vile viwango tofauti vya riba, pointi au ada.

Ishara zinazowezekana za Ubaguzi

“Tangazo lina kosa. Kuanzia Agosti kodi itaongezeka kwa $50 kila mwezi.”

“Huwa tunakubali watu wanaozungumza kiingereza vyema pekee.”

“Unaweza kuwa na starehe zaidi ukiishi mahali pengine. Nitakuonyesha ujirani ulio na misikiti.”

“Kwa bahati mbaya, tuna ngazi tu. Hatuwezi kukubali matumizi ya kifaa cha kutembea kwa ajili yako.”

“Kuna trafiki nyingi sana katika eneo hili. Si salama kwa watoto kuishi hapa.”

“Tunapendekeza wewe na familia yako kukodisha katika ghorofa ya kwanza kwa ufikiaji rahisi.”

“Kwa bahati mbaya, ukarabati wa choo na vifaa vya kufua haupatikani hadi wiki ijayo.”

“Samahani, hiki ni chumba cha mtu mmoja.”

“Kutokana na asili yako, tutahitaji kuchukua hati za ziada.”

“Mbwa hawaruhusiswi katika jengo hili, hili haliwezi kubadilishwa.”

“Fleti niliyokwambia kuhusu wakati wa simu yetu imepangishwa tayari.”